



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Unapojibu tafadhali taja:

KUMB.NA. E.169/210/01/04

17, Julai 2023

Yah: TANGAZO LA UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU

Husika na mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea barua yenye Kumb Na.BA.87/226/01A/50 ya tarehe 28 Aprili 2023 kutoka kwa katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza juu ya uanzishwaji wa Bodi ya mfuko wa Elimu kutokana na barua hiyo Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela anawatangazia Wananchi wenye sifa na wanaoishi Mnisppaa ya Ilemela, kuomba nafasi mbalimbali ili kuunda Bodi ya mfuko wa Elimu wa Manispaa. Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo.

- Mwenyekiti.
- Wawakilishi wawili wa jamii ambapo mmoja kati yao lazima awe mwanamke.
- Mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa wakuu wa Shule za Sekondari zilizopo katika eneo la Halmashauri.
- Mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa Walimu wakuu wa Shule za Msingi zilizopo katika eneo la Halmashauri.
- Mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa wamiliki wa Shule zisizo za Serikali; na
- Diwani mmoja kutoka kamati ya huduma za jamii ya Halmashauri

Sifa za wajumbe wa Bodi

- Awe ni raia wa Tanzania isipokuwa tu kama mjumbe husika anatokea katika shirika lisilokuwa la kiserikali.
- Awe na Umri usiopungua miaka ishirini na moja.
- Awe na akili timamu.
- Awe na Elimu ya Sekondari na kuendelea
- Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha siasa isipokua tu kwa Diwani anaye wakilisha kamati ya huduma za jamii ya Halmashauri
- Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu ukosefu wa uaminifu; na
- Awe mkazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa Ilemela, 200 Br. ya Buswelu, 33282 Buswelu,
S.L.P 735 Ilemela, Mwanza. Simu: + 255 (28) 2981196, Nukushi: + 255 (28) 2981196,
Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz Tovuti: www.ilemelamc.go.tz
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 28 Julai, 2023 na barua zote zitumwe kwa Anwani ifuatayo

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P 735,
ILEMELA – MWANZA



Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa Ilemela, 200 Br. ya Buswelu, 33282 Buswelu,
S.L.P 735 Ilemela , Mwanza. Simu: + 255 (28) 2981196, Nukushi: + 255 (28) 2981196,
Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz Tovuti: www.ilemelamc.go.tz
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)